# KISWAHILI

## Kitabu cha Nne

# 斯瓦希里语

第四册

沈志英　章培智　申 钧　编著

外语教学与研究出版社

¥: 22.90
ISBN 7-5600-0640-X
9 787560 006406 >

一个学术性教育性
出版机构

网址：http://www.fltrp.com

# KISWAHILI

## Kitabu cha Nne

# 斯瓦希里语

## 第四册

沈志英　章培智　申　钧　编著

外语教学与研究出版社

(京)新登字155号

责任编辑：沈志英
责任校对：章培智　申　钧

斯瓦希里语
（第四册）
沈志英　章培智　申　钧　编著

*　*　*
外语教学与研究出版社出版发行
（北京西三环北路19号 100089）
http://www.fltrp.com
北京外国语大学印刷厂印刷
开本 850×1168　1/32　17.25印张　276千字
1991年6月第1版　2003年10月第2次印刷
印数：1501—1800册
*　*　*
ISBN 7-5600-0640-X
G·306
定价：22.90元

# 前　　言

本书是斯语基础阶段的最后一册书，也是向提高阶段的过渡、用作承上启下的教材。为此，我们在编写过程中，既考虑到要进一步巩固前几册所学过的基本知识和基本技能，也要为学生进入提高阶段作一些必要的准备。

在编写中，我们作了如下安排：

1．选材范围较广。大部分选自东非不同斯语国家所编写的资料，是在对其内容和体系等方面进行了一定研究的基础上，经过筛选而采用的，旨在使学生对各地区斯语的不同流派、语言风格特色和表达方法有一定的了解。对一些经过十几、二十几年的教学实践证明有适用性价值的教材，在选用时也作了某些筛选、删改等去粗取精的加工。

2．题材、内容多样化。课文内容涉及到斯语国家的政治、历史、经济、文化风俗、宗教信仰等概况和背景知识，具有较好的知识性和可读性。

3．语言有一定的深度。个别课文无论在词语运用或句子构成上，都有较丰富的表达形式。此外，在 "Kiswahili Sanifu" 中，例举了更多的常用词组搭配形式和习惯用语，有助于提高学生灵活运用语言的能力。除了课文中出现的斯语句型、习惯用语等外，课文后均增加了两条常用谚语，要求学生必须牢记掌握。

4．增加了练习部分的难度。练习量大，内容多，形式新，进一步加强了阅读理解、翻译写作、综合归纳等实践能力的培养和训练，便于学生顺利地进入提高阶段。

此为试读，需要完整PDF请访问：www.ertongbook.com

# YALIYOMO

Somo la Kwanza .................................. 1
Somo A: Kalenda
Somo B: Kalenda ya Kiswahili

Somo la Pili .................................. 25
Somo A: Kazi ni Uhai
Somo B: Nani Mwenye Kazi Zaidi ya Wengine ?

Somo la Tatu .................................. 47
Somo A: Mwanamke Amkabili Mzuka
Somo B: Kisa cha Jina Langu

Somo la Nne .................................. 68
Somo A: Kuepuka Hatari kwa Shida
Somo B: Maafa ya Uvuvi

Somo la Tano .................................. 90
Somo A: Hakuna Siri ya Wawili Duniani
Somo B: Ujuzi Na Uvumbuzi

Somo la Sita .................................. 117
Somo A: Mikasa ya Dunia
Somo B: Maajabu ya Ulimwengu Hayana Mwishio

Somo la Saba .................................. 141
Somo A: Urembo wa Ndonya
Somo B: Kawambwa Na Makapu ya Karanga

Somo la Nane .................................. 162
Somo A: Chambo cha Pesa

Somo B: (1) Fimbo ya Ulimwengu
(2) Kukopa Arusi-Kulipa Matanga

Somo la Tisa .................................. 187
Somo A: Tufai
Somo B: Roho Mkononi

Somo la Kumi .................................. 210
Somo A: Mashindano ya Mpira wa Miguu
Somo B: Kushindwa Kwa Tanzania Los Angeles

Somo la Kumi Na Moja .......................... 234
Somo A: Safari ya Beijing
Somo B: Kuanguka kwa Theluji

Somo la Kumi Na Mbili .......................... 262
Somo : Majira ya Baridi ya Beijing

Somo la Kumi Na Tatu .......................... 288
Somo A: Mbuga ya Wanyama ya Ziwa Manyara
Somo B: Safari Yangu Katika Mbuga ya Wanyama ya Mikumi

Somo la Kumi Na Nne .......................... 319
Somo A: Mlima Kilimanjaro
Somo B: Paa la Afrika

Somo la Kumi Na Tano .......................... 350
Somo A: Mavazi Kwa Jumla
Somo B: Mapishi -- Chakula Bora

Somo la Kumi Na Sita .......................... 379
Somo A: Ninavyoielewa Dini ya Uislamu

Somo B: Dini ya Asili

Somo la Kumi Na Saba .......................... 413
Somo A: Michezo ya Sarakasi
Somo B: Ustadi wa China Katika Michezo ya Sarakasi

Somo la Kumi Na Nane .......................... 446
Somo : Habari za Wasanifu Mashuhuri Waliojitokeza Kuipamba Lugha ya Kiswahili

Somo la Kumi Na Tisa .......................... 472
Somo : Matokeo

Somo la Ishirini .............................. 496
Somo : Mkulima Jasiri

# SOMO LA KWANZA

| |
|---|
| Somo A: Kalenda |
| Somo B: Kalenda ya Kiswahili |

## SOMO A

### Kalenda

Eti leo ni siku gani ? Au, leo tarehe ngapi ati ? Au, mwezi gani huu ? Tukitaka kuyajibu maswali kama hayo hatuna budi kuikodolea macho kalenda.

Masimulizi kuhusu kalenda yetu yanaanzia mbali sana wakati wa macheo ya ustaarabu. Wahenga na wahenguzi wetu walibashiri wakati kutokana na macheo na machweo ya jua. Leo hivi zipo jamii fulani zinazofuata utaratibu huo wa kubashiri wakati. Siku kama tunavyoielewa ni vile vipindi vya kutwa na kuchwa pamoja; laki-

ni kwa muda mrefu watu wa kale hawakuelewa maana ya siku kama sisi leo tunavyoielewa.

Yumkini mara tu watu walipoanza kuhesabu siku waliyaona mabadiliko kwenye mwezi. Wakati fulani mwezi ulikuwa mpevu; kisha ulianza kuwa mdogo mdogo hata hatima yake ukatoweka. Halafu kuchwa kucha, kuchwa kucha, mwezi mwandamo uliendelea kukua kama uyoga hadi kufikia kikomo chake cha kuwa mwezi mduara.

Kipindi toka mwezi mpevu hadi kufikia mwezi mpevu mwingine kilikuwa kipindi kizuri cha kuweza kuupima wakati. Hata hivyo kilikuwa kipindi kifupi mno watu kuweza kukitumia kama msingi wa kalenda.

Baadaye watu waliona kuwa majira fulani yalifuatana kwa utaratibu maalumu. Kwa mfano, katika Misri ya kale, majira ambayo mto Nile ulifurika na kuyagharikisha makonde yalifuatiwa na majira ya kupanda mazao. Baadaye yalifuata majira ya kuvuna. Mzunguko huu wa majira ulichu-

kua kipindi cha mwaka mzima.

Japo kilikuwa ni kipindi kirefu hata hivyo hapakuwepo mtu aliyediriki kuziweka pamoja siku na miezi katika kipindi kizima cha mwaka. Hata baadhi ya wale watu waliojaribu waliishia kwenye matatizo chungu nzima. Sababu yenyewe ni kuwa siku haziingiliani vema katika miezi; kwa sababu kipindi kati ya mwezi mpevu na mwezi mpevu mwingine kina siku 29.5. Waaidha siku katika mwaka haziingiliani vema kwa kuwa safari ya sayari ya dunia katika kulizunguka jua huchukua siku kama 365, saa 5 dakika 49 na sekunde 46. Hata hivyo bado tatizo hilo linaendelea kwa sababu miezi yenyewe haiingiliani vema katika miaka kwa sababu mwezi huizunguka dunia kati ya safari 12 na 13 kwa mwaka.

Makahini wa Babiloni ya kale walitengeneza kalenda yenye siku 29 kwa baadhi ya miezi na siku 30 kwa miezi mingineyo. Kwa kawaida mwaka wa Wababiloni ulikuwa na miezi 12. Hata hivyo kalenda hiyo ya



此为试读，需要完整PDF请访问：www.ertongbook.com

mwaka ilionyesha dosari kwa sababu mwaka ulikuwa na upungufu wa siku kadhaa.

Upungufu huu ulisababisha siku na miezi ichopoke upesi upesi toka kwenye majira. ( Kalenda hiyo ingeruhusiwa kuendelea kutumika na upungufu wake huo mwaka ungekuwa na upungufu wa siku kadhaa ukilinganisha na idadi ya siku ambazo dunia inachukua kumaliza safari ya kulizunguka jua. Yasemekana upungufu huo ungeruhusu majira ya baridi kali mzizimo yatokee katikati ya mwezi Oktoba kila baada ya miaka 20. ) Makahini hao wakijaribu kuzuia miezi isichopoke majira haraka haraka, waliongeza mwezi mmoja zaidi kwenye kalenda, kila baada ya miaka kadhaa. Kalenda hiyo yashabihiana sana na kalenda ya mwezi ya Kichina.

Wágiriki na Warumi wa kale walikuwa na kalenda zilizofanana na kalenda ya Wababiloni. Ila wakati Juliasi Kaisari alipokuwa mtawala wa dola ya Warumi, kalenda hiyo ya Kirumi ilikuwa imeburugika mno

kwa matumizi bora. Kwa hiyo Kaisari akaamua kuitupilia mbali na kutengeneza nyingine kwa upya kabisa. Alimtafuta mnajimu maarufu ili amshauri katika kazi hiyo. Mnajimu wake Sosigenes alishauri kuwa urefu wa mwaka uwe siku 365.25 . Kaisari akatoa agizo kuwa mwaka uwe na siku 365, na kila baada ya kipindi cha miaka minne siku moja iongezwe kwenye mwisho wa mwezi Februari ili kuongezea jumla ya robo siku nne zilizopotea katika kipindi hicho cha miaka minne.

Ili kuhakikisha kuwa kalenda yake ilifuata majira kamili ya mwaka, Kaisari aliiondoa sikukuu ya mwaka mpya toka tarehe mosi March na kuiweka kwenye Januari mosi.

Mabadiliko hayo yaliufanya mwezi Januari kuwa mwezi wa kwanza wa mwaka. Majina ya miezi yalibakia kama yalivyokuwa katika kalenda za zamani. Kutobadilika kwa majina ya miezi katika kalenda ya Julius Kaisari, kumesababisha mwezi wa

tisa wa mwaka uwe na jina Septemba, maana yake hasa ikiwa ni saba. Tena majina ya miezi ya kumi, ya kumi na moja na ya kumi na mbili yanayo dosari hiyo hiyo ya mwezi wa tisa. Kwa sababu Oktoba, Novemba, Desemba ni maneno ya Kilatini yenye maana ya nane, tisa na kumi.

Mnajimu wa Kaisari, Sosigenes aliamua kuugawa mwaka katika miezi 12 yenye karibu siku sawa. Mpango huo uliupatia mwaka miezi 5 yenye siku 31 na miezi 7 yenye siku 30. Warumi wa kale walionelea kuwa nambari witiri zilikuwa na sudi kwa hiyo wakaichukua siku moja toka mwezi Februari ambao hadi hapo ulikuwa na siku shufwa 30, na kuipachika siku hiyo kwenye mwezi mwingine ili tu uwe na nambari witiri yaani siku 31.

Aidha Juliusi Kaisari aliupa mwezi mmoja jina lake kwa heshima yake ndio mwezi Julai na sawia akiuongezea siku moja ya ziada ili upate kuwa na siku witiri 31.

Juliusi Kaisari aliipa dunia mkono wa buriani na kiti chake kikakaliwa na Augustus Octavian. Augustus Octavian kama Juliusi aliupa mwezi mmoja jina lake kwa heshima yake. Ndio mwezi Agosti. Augustus Octavian hakuweza kuhimili kuona mwezi uliopewa jina na Juliusi ukiwa na hesabu witiri siku 31 na ambapo mwezi wake ulikuwa na siku moja pungufu. Kwa hiyo akaichukua siku nyingine toka mwezi Februari na kuiongeza kwenye mwezi wake Agosti ili uwe na urefu sawa na mwezi Julai.

Baada ya mabadiliko hayo kulikuwepo sasa miezi 7 yenye siku 31 katika mwaka, ila mwezi Februari ulibakiwa na siku 28 tu, na kuzidi kidogo kwa miaka mirefu. Tangu hapo hadi leo majina ya miezi yamebakia bila mageuzo yoyote.

Utaratibu uliowekwa na watawala hao wawili kuhusu miaka mirefu uliendelea bila mabadiliko hadi mwaka 1600. Hadi kufikia mwaka huo wa 1600 dosari ya siku 10 zilizojilimbikiza ilijidhihirisha. Ta-

tizo hili lilitokea kwa sababu ilibainika kuwa mwaka haukuwa na siku 365.5 kama alivyosema mnajimu Sosigenes. Kwa mfano watu walipouongezea mwezi Februari siku moja kila baada ya miaka minne walifanya kosa la kuongeza saa 24 badala ya kuongeza saa 5 x 4; dakika 48 x 4; sekunde 46 x 4. Dosari yenyewe ilikuwa na ziada ya dakika 44 na sekunde 56 kwa kila mwaka mrefu au dakika 11 na sekunde 14 kwa kila mwaka mfupi.

Dosari hiyo ikiangaliwa kwa juu juu si kubwa ya kutisha lakini unapozidisha dosari hiyo kwa muda wa miaka 1600, kosa la dosari hiyo linatisha ajabu.

Ni kutokana na dosari hiyo ndipo mwaka 1582 Papa Mtakatifu Gregori wa XIII kwa kuzingatia ushauri wa mnajimu wa Kiitaliano Clavius, alipoamuru kuwa siku 10 ziondolewe katika mwaka. Papa Mtakatifu Gregori wa Kumi Na Tatu, pia alimtaka mnajimu Clavius kutengeneza utaratibu bora wa miaka mirefu ambao haungesababi-

sha kujilimbikiza kwa siku hapo baadaye. Clavius aliutengeneza utaratibu wa kijanja ambao hata sisi hivi leo twaufuata.

Japokuwa kalenda ya Gregori ilionekana sahihi sana, lakini ilikuwa na dosari ya ziada ya sekunde 26. Kwa muda wa miaka 3000 kalenda hiyo itakuwa imejilimbikizia siku moja zaidi ya saa 24.

Nchi zote za kikatoliki zilikubali mara moja kalenda ya Gregori, ila kanisa la kigiriki na baadhi ya mataifa ya dini za kiprotestanti waliibeua kalenda hiyo.

Ilikuwa ni baada ya miaka 200 nchi ya Uingereza ilipoamua kuondoa siku 11 kwenye mwaka ili kufanya kalenda kuwa imara. Tendo hili lilifanyika kwa sheria ya bunge la mwaka 1752, lakini wananchi wengi waliipinga sheria hiyo wakilalamika kuwa sheria hiyo ilikuwa inawapunguzia siku 11 katika maisha yao.

Kulikuwepo mikutano mingi baada ya sheria hiyo kupitishwa kuipinga hiyo sheria. Watu wengi walipiga mayowe katika



此为试读，需要完整PDF请访问：www.ertongbook.com